BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 10 Juni, 2017.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

MASWALI:

Ofisi ya Rais, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

61. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Kwa kuwa eneo la nyuma ya Ikulu linapakana na eneo la bahari.

Je, Serikali imefikiria kumtengenezea Jahazi Maalum Mhe. Rais kwa ajili ya wageni wanaomtembelea.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

183. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

Hivi karibuni kumetokea kadhia ya wananchi maeneo ya Wilaya ya Kati kuvunjiwa nyumba zao kwa madai

kuwa wamejenga katika maeneo ya eka ambayo hayaruhusiwi kufanywa makaazi. Hata hivyo, inaonekana kuwa tatizo hilo linasababishwa na taasisi za Serikali kushindwa kuchukuwa hatua mapema tokea wananchi hao wanapoanza ujenzi badala yake wanasubiri mpaka wananchi wanamaliza kujenga na ndipo hatua za kubomolewa zinafuata.

(a) Je, kwanini Serikali inachelewa kuchukuwa hatua kwa wanaojenga maeneo yasiyoruhusiwa na badala yake wanasubiri mpaka wamalize ndipo wabomowe.

(b) Kwa kufanya hivyo, Wizara haioni kuwa inawachonganisha wananchi na Serikai yao kuona inawaonea.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

173. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Zanzibar imekuwa na vijana wengi wanaomaliza vyuo vikuu katika fani mbali mbali, lakini vijana hao wanapomaliza wanakosa fursa za ajira. Lakini cha kusikitisha Serikali imekuwa ikiwaongezea mikataba ya ajira wafanyakazi ambao wameshafikia umri wa kustaafu wakati vijana wa kushika nafasi hizo wapo na wananyimwa ajira kwa kisingizio cha uzoefu na umri na uchache wa nafasi za ajira.

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea watu waliostaafu kupewa mikataba ya kazi wakati vijana wanaomaliza vyuo katika fani hizo wapo.

(b) Kuna watu wangapi wameongezewa mikataba ya ajira na fani zao ni zipi.

(c) Kuna tathmini gani imefanywa kujua vijana ambao hawana ajira na fani zao ni zipi.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

112. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi kutoa huduma na mafunzo kwa Bibi na Bwana shamba ili eneo dogo litumike na kupata mazao mengi zaidi. Hata hivyo, Wizara hii ina maeneo mengi inayoyamiliki lakini maeneo hayo yamesahaulika.

(a) Kwa kuwa wao ni wataalamu wa kilimo (Bibi na Bwana shmba) kwa nini hawaoneshi mfano wa uzalishaji bora katika mashamba hayo.

(b) Kwa kuwa Wizara hii ina dhamana ya chakula hapa Zanzibar, kwa sasa nchi ipo asilimia ngapi kufikia kujitosheleza kwa chakula.

(c) Mchele ndio chakula kikuu, ni lini Zanzibar itajitosheleza kuzalisha mchele wa aina tofauti.

Wizara ya Fedha na Mipango:

102. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa muda mrefu Zanzibar kumekuwa na kilio cha kuanzishwa kwa Baraza la Rufaa za Kodi, na bahati nzuri ni kuwa Baraza hilo limeshaanzishwa. Hata hivyo, hivi sasa kumekuwa na tatizo la kutokuwepo kwa Kanuni za kuendesha mashauri ya Baraza hilo wakati tayari Baraza hilo linafanyakazi, Mwenyekiti wake ameshateuliwa na anaendelea kusikiliza mashauri mbalimbali yanayofika kwake.

Je, ni sababu gani zimepelekea mpaka hivi sasa kutokuwepo kwa Kanuni za uendeshaji mashauri ya Baraza hilo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

108. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Zanzibar ni nchi moja wapo ambayo wananchi wake wanatumia usafiri wa vyombo vya maringi mawili kama vespa, pikipiki na kadhalika. Vyombo hivyo hutumika kwa watu wenye rika tofauti ambapo kwa sasa hutumika kwa vijana kuanzia miaka kumi na tano. Na vijana hao hutumia zaidi vyombo hivyo kwa fujo kwa kwenda mbio kupita kiasi ambapo huhatarisha maisha yao na maisha ya watumiaji wengine wa barabara hizo.

(a) Je, Serikali hailioni tatizo hili.

(b) Kama inalijua, hatua gani zimechukuliwa kukomesha vitendo hivyo.

(c) Ni lini Serikali itapiga marufuku vitendo hivyo ili kupunguza ajali.

149. MHESHIMIWA DKT. MWINYIHAJI MAKAME MWADINI (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Imekuwa kawaida siku hizi kwa wanafunzi wa udereva kujifunza katika viwanja vya Maisara.

(a) Kwanini Wizara yako inaliachia suala hilo kuendelea na kuharibu viwanja vya michezo.

(b) Hatua gani Wizara yako itachukua kudhibiti vitendo hivyo.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

88. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Hivi karibuni Zanzibar imeshuhudia nguvu mpya ya kuimarisha soka Zanzibar baada ya kuanza mashindano ya Majimbo (Majimbo Cup) ambayo yalifunguliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein. Katika uzinduzi wake Mhe. Rais alipongeza Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuyafadhili mashindano yale ambayo yeye mwenyewe ni Mwenyekiti.

(a) Je, mbali na mkakati huu mzuri wa kuimarisha soka visiwani, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mpira wa miguu Zanzibar unapiga hatua katika ngazi zote za ligi.

(b) Je, kwa vile muda mrefu kumekuwa na matatizo ya uongozi katika vyama vya mchezo wa soka Zanzibar, Serikali haioni ni muhimu sasa kuwaita wahusika wote na kukaa nao pamoja na wataalamu mbali mbali ili kuweka dira ya mchezo wa mpira wa miguu hasa katika uongozi.

185. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Uwanja wa Gombani ni miongoni mwa viwanja vizuri vya mpira wa Miguu nchini na hivi karibuni umewekwa nyasi bandia na mpira wa kukimbilia. Hata hivyo, ubao wa kusomea magoli (score board) umekuwa katika hali mbaya na unaleta taswira mbaya katika vitu vingi vizuri vya uwanja huo.

Je, Serikali inajipangaje katika kujenga ‘score board’ ya kisasa Gombani kama ile ya Uwanja wa Amani ili kuimarisha taswira nzuri ya uwanja.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

175. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hivi karibuni kumekuwa na taarifa za kuongezeka vitendo vya kupata mimba wanafunzi ambavyo vinaathir maendeleo ya wanafunzi hao Unguja na Pemba.

Je, ni wanafunzi wangapi wamepata mimba Unguja na Pemba na Wizara imechukuwa hatua gani kwa wanafunzi hao.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

171. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wafanyakazi wa kituo cha kulea watoto cha Mazizini kuwa Mkuu wa Kituo hicho amekuwa anatumia lugha mbaya kwa wafanyakazi waliopo hapo na kurudisha nyuma morali ya kazi ya watumishi hao.

Je, Wizara haioni kuwa jambo hili linaleta kasoro ya kiutendaji kwa wafanyakazi wa kituo hicho muhimu kwa malezi ya watoto.

Wizara ya Afya:

179. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Waziri wa Afya:

Mara kadhaa Hospitali ya Mnazimmoja imekuwa inakumbwa na tatizo la uhaba wa maji na siku nyengine yanakosekana kabisa. Mfano mzuri ni hivi karibuni ambapo maji yalikosekana na Uongozi wa Hospitali ukakanusha licha ya kuwepo ushahidi kuwa maji yalikosekana.

(a) Je, Kwanini Hospitali kubwa ya rufaa ya Mnazimmoja haina mfumo wa maji endelevu na badala yake inatokea kukosa maji.

(b) Mpango wa kugawa maji ya zamu kwa Hospitali ya Mnazimmoja si kuhatarisha maisha ya wagonjwa.

(c) Uongozi wa Hospitali kukanusha taarifa za uhaba wa maji, si kuweka rehani maisha ya wananchi wetu.

Zanzibar,
10 Juni, 2017.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.